

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SITA

24 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 24 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

179. MHESHIMIWA DKT. REGINA CHRISTOPHER MALIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa muda mfupi na wa kati wa kupunguza changamoto ya ajira kwa Vijana hususani Wahitimu wa Vyuho Vikuu.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

180. MHESHIMIWA SALUM KHAMIS SALUM (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko la Mnada wa Mifugo ili kuwa na Soko lenye hadhi na kuongeza mapato ya Halmashauri katika Jimbo la Meatu.

181. MHESHIMIWA OMARY MARCUS MSIGWA (MADABA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaongeza Watumishi wa Sekta ya Afya wakiwemo Wataalamu wa Mionzi katika Jimbo la Madaba.

WIZARA YA UCHUKUZI:

182. MHESHIMIWA HASNAIN GULAMABBAS DEWJI (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kwa Wananchi wa Kilwa Masoko waliopisha upanuzi wa eneo la Uwanja wa Ndege.

WIZARA YA MAJI:

183. MHESHIMIWA TINNAR ANDREW CHENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani kufikisha huduma ya Maji Safi na Salama kutoka Ziwa Victoria kwa Wananchi wanaoishi umbali zaidi ya Km 12 kutoka Bomba Kuu.

184. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Miji 28 ya Rorya – Tarime utakamilika.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

185. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kufufua Viwanda vilivyotelekezwa muda mrefu ili kuleta ajira kwa watu wa Musoma.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

186. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufuatilia maendeleo ya Wanafunzi wanaofanya vizuri kitaifa ili kuhakikisha wanakuwa rasilimali muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

WIZARA YA FEDHA:

187. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaanzisha Mkoa wa Kikodi katika Wilaya ya Karatu.

WIZARA YA UJENZI:

188. MHESHIMIWA HAMOUD ABUU JUMAA (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali italipa fedha za kuanza kazi kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Mlandizi hadi Ruvu SGR *Station* ili ujenzi uanze rasmi.

189. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara kutoka Makongolosi hadi Rungwa utaanza.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

190. MHESHIMIWA MARY DANIEL SURATI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fidia kwa wakati kwa Wananchi walioathiriwa na Wanyamapori.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA
24 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**